TMIF UPDATES

Tanzania Mining and Investment Forum 2023

25TH OCTOBER 2023

www.madini.go.tz | Ministry of Minerals | Special Online Edition

SERIKALI KUENDELEA KUWEKA MAZINGIRA RAFIKI SEKTA YA MADINI

Na Wizara ya Madini- DSM

Serikali imewahakikishia Wawekezaji Wakubwa , Wa kati na Wa dogo katika Shughuli za Madini nchini kuwa itaendelea kuweka mazingira rafiki na wezeshi katika mnyororo mzima wa Sekta ya Madini kama Sera ya Madini ya Mwaka 2009 inavyoelekeza.

Hayo yamebainishwa Oktoba 25, 2023 na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Dkt.Doto Biteko akimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt.Samia Suluhu Hassan katika Ufunguzi wa Mkutano wa Kimataifa wa Madini na Uwekezaji Tanzania 2023 jijini Dar es salaam lenye kauli mbiu inayosema " Kuifungua Tanzania katika Fursa za Uwepo wa Madini"

Dkt.Biteko amesema kuwa Serikali ipo kwenye mpango wa kufanya utafiti wa kina wa jiofizikia katika eneo lote la nchi ili kupata taarifa za aina ya miamba na madini yaliyopo ili kuwepo na Kanzidata ya taarifa itakayosaidia katika utafiti wa kina.

Dkt. Biteko amefafanua kuwa kuwepo kwa taarifa za utafiti kutawezesha kufungua migodi zaidi pamoja na kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi kwa kufungamanisha sekta ya madini na sekta nyingine za kiuchumi kama vile Maji na Kilimo.

Akielezea kuhusu uboreshaji wa miundombinu katika migodi mikubwa na midogo Dkt.Biteko ameeleza kuwa tayari mitambo mitano ya Uchorongaji miamba kwa wachimbaji wadogo imekabidhiwa na ifikapo mwezi juni 2024 mitambo mingine kumi itakabidhiwa.

Dkt.Biteko ameongeza kuwa mpaka sasa zaidi ya migodi 360 ya wachimbaji wadogo imeunganishwa na Nishati ya Umeme pamoja na kampuni kubwa 9 zimeingia ubia na Serikali katika utafiti na uchimbaji madini ya kimkakati yakiwemo madini ya Nikeli, Kinywe , Makaa ya Mawe.

Awali , Waziri wa Madini Mhe.-Anthony Mavunde ameeleza kuwa Mkutano huu wa mwaka 2023 unatoa fursa kwa kampuni za madini kujadili kuhusu taarifa za namna ya upatikanaji wa mitaji , Utafiti , Uchimbaji na Uchenjuaji na uwekezaji kwa kuzingatia mazingira rafiki baina ya Serikali na Taasisi na Kampuni binafsi.

Akizungumzia kuhusu umuhimu wa taarifa za jiolojia Mhe.Mavunde amesema uwepo wa taarifa za utafiti wa jiolojia na Jiofizikia kutawezesha kujua

aina ya mashapo yaliyopo na kuchimba kwa uhakika na kuwepo kwa uwekezaji wenye uwiano sawa baina ya Serikali na Wadau wa Sekta ya Madini hasa katika uvunaji madini kibiashara.

Kwa upande wake , Waziri wa Madini kutoka nchi ya Mhe.-Monica Chang'anamuno (MP), amesema kuwa anaamini kupitia jukwaa hili atajifunza mengi juu ya mipango ya maendeleo ya sekta ya madini nchini Tanzania hasa kwenye madini ya Kimkakati na madini adimu.

Aidha , akielezea kuhusu mikakati ya Serikali ya Malawi kupitia Vision ya 2036 , ameeleza kuwa Serikali ya Malawi imefanikiwa kufanya utafiti wa Jiolojia kwa asilimia 80 na kugundua madini mbalimbali yakiwemo madini kimkakati na madini adimu (Rare Earth Elements) ambayo yote yapo katika mpago wa uwekezaji.

Akielezea kuhusu utafiti wa kina Waziri wa Madini wa Uganda Mhe . Lukeris amesema jiolojia ya Afrika inatofautiana kidogo hivyo ni muhimu kufanya utafiti wa kina ili kubaini wingi na ubora wa madini yaliyopo katika sehemu husika kuwepo kwa taarifa za namna hiyo kutarahisisha kuvutia wawekezaji bila kuhangaika na upembuzi yakinifu.

Akielezea mkakati wa sekta ya madini nchini Uganda Waziri Mhe. Peter Lukeris (MP) amesema kwasasa Serikali ya Uganda kwa kushirikiana na sekta binafsi inaendelea na ukusanya wa taarifa za kina kwenye Madini na Mafuta ili kupata sahihi za uwekezaji.

Kuhusu umuhimu wa kuwepo kwa utafiti wa Nishati ya Umeme kupitia madini ya Uraniam , Mhe.Waziri Lukeris amezitaka Serikali za Afrika kuanza kufikiria kuzalisha Nishati umeme kupitia madini ya Uraniam kama Uganda ilivyoanza.

Naye, Katibu Mkuu Wizara ya Madini Kheri Mahimbali akifungua Jukwaa ameeleza kuwa jukwaa hili ni sehemu ya Utekelezaji wa Sera ya Madini ya Mwaka 2009 yenye lengo la kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Madini kwa kufanya majadiliano na kutoa mapendekezo ya namna gani ya kuboresha Sera ya Madini ya Mwaka 2009.

Akielezea maendeleo ya Sekta ya Madini , Mahimbali amefafanua kuwa Sekta imeendelea kukua ambapo kwasasa katika Pato la Taifa inachangia asilimia 9.1 kwa mwaka 2022.

Kwa upande wa kutoa ajira sekta ya Madini kwa mwaka 2021 ilitoa ajira 14308 na Mwaka 2022 kiwango kiliongezeka mpaka kufikia 16462.

Sambamba na hapo kuna ongezeka la mauzo ya bidhaa zitokanazo na madini mfanokwa mwaka 2021 mauzo yalikuwa bilioni 3.1 kwa mwaka 2022 yameongezeka kufikia mwaka 3.4.

SERIKALI KUENDELEA KUWEKA MAZINGIRA RAFIKI SEKTA YA MADINI

Imeelezwa kuwa, Sekta ya Madini ni nguzo muhimu na chachu ya maendeleo ya uchumi wa nchi kupitia rasilimali madini iliyopo nchini.

Hayo yameelezwa Oktoba 25, 2023 na Naibu Waziri Mkuu ambaye pia ni Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko alipomwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Ufunguzi wa Jukwaa la Madini na Uwekezaji Tanzania 2023 jijini Dar es salaam.

"Kutokana na umuhimu wa Sekta ya Madini katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kuvutia uwekezaji zaidi," amesema Dkt. Biteko

Amesema kuwa, Sekta ya Madini inafungamanishwa na Sekta nyingine za Kiuchumi kama vile viwanda na kilimo ili kuzalisha bidhaa mbalimbali zinazotumia madini kama malighafi mfano mbolea, betri za magari, simu, kompyuta na bidhaa nyingine.

"Niwahakikishie kuwa, mazingira ya uwekezaji katika Sekta ya Madini yameendelea kuboreshwa na kuwa rafiki zaidi. Nafurahi kusema kuwa, hadi sasa jumla ya Kampuni tisa za Kimataifa za uchimbaji mkubwa wa madini zimeingia ubia na Serikali katika uchimbaji wa madini mbalimbali ikiwemo madini ya nikeli, kinywe, heavy mineral sands (mchanga bahari), Rare Earth Elements, dhahabu na almasi," ameongeza Dkt. Biteko

Aidha, Serikali inaendelea kuhakikisha kuwa miundombinu mbalimbali inaboreshwa ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa umeme wa uhakika pamoja na ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji.

Kwa upande wake, Waziri wa Madini, Mhe. Anthony Mavunde amesema kuwa ili kuhakikisha nchi ya Tanzania inanufaika na rasilimali madini, Wizara

itaendelea kuimarisha usimamizi wa shughuli za Sekta ya Madini ili kuhakikisha inawanufaisha wananchi na Serikali inapata mapato stahiki.

"Wizara itaendelea kuimarisha usimamizi wa shughuli za Sekta ya Madini ili kuhakikisha kuwa mchango wake unakua hadi kufikia asilimia 10 ya Pato la Taifa kufikia mwaka 2025 kama ilivyo katika Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025. Tutashirikiana na wadau mbalimbali wa Sekta kuhakisha lengo hilo linafikiwa," ameongeza Waziri Mavunde.

Kwa upande mwingine, Mawaziri wa Madini kutoka nchini Malawi Mhe. Monica Chang'anamuno na Mhe.Peter Lokeres kutoka nchini Uganda wamesema kuwa Afrika ina fursa nyingi za Sekta ya Madini zinazovutia wawekezaji kuwekeza.

Mkutano wa Madini 2023 umehudhuriwa na mawaziri kutoka nje ya nchi, Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Nishati na Madini, Makatibu Wakuu na Manaibu Wakuu kutoa Tanzania Bara na Visiwani, Waheshimiwa Mabalozi, Viongozi wa Serikali, Vyama vya siasa na Wakuu wa Taasisi.

SERIKALI YAJIPANGA KUFANYA TAFITI ZA KINA KUPITIA VISION 2030

Kutokana na umuhimu wa shughuli za kina za utafiti wa madini katika maendeleo ya Sekta ya Madini, akizungumza wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa KImataifa wa uwekezaji katika Sekta ya Madini, Waziri wa Madini Dkt. Doto Biteko amesema Ili kutekeleza mpango wa upatikanaji wa taarifa za kijiolojia, Wizara imekuja na kaulimbiu isemayo "Vision 2030, Madini ni Maisha na Utajiri".

Ameongezakwamba, Kaulimbiu hiyo inalenga kutumia rasilimali madini kubadili hali ya maisha ya Watanzania kwa kuimarisha vipato vyao kupitia shughuli za uchimbaji wa madini na Sekta nyingine za kiuchumi kufungamanishwa na Sekta ya Madini kwa maendeleo endelevu ya uchumi wa Taifa.

Ili tuweze kutumia rasilimali tulizonazo kufikia lengo hilo, tuweze kutumia rasilimali tulizonazo kufikia lengo hilo, tunahitaji kupata taarifa za kijiolojia katika maeneo mbalimbali ya nchi zitakazowezesha kugundua mashapo ya kuanzisha miradi ya madini.

Mhe. mgeni rasmi, Ili kupata taarifa za kijiolojia, Wizara imepanga kufanya utafiti kwa teknolojia ya kisasa "High Resolution Airborne Geophysical Survey" katika eneo kubwa zaidi nchi nzima ifikapo mwaka 2030".

Ameongeza kwamba, upatikanaji wa taarifa za kijiolojia katika maeneo mengi ya nchi yetu utahamasisha kasi ya uwekezaji katika utafutaji wa kina wa madini nchini ambao ndio msingi mkubwa wa uanzishwaji wa migodi.

MHE. MAVUNDE ATETA NA BALOZI WA KANADA NCHINI TANZANIA

Waziri wa Madini Mhe.Anthony Mavunde amezungumza na Balozi wa Kanada Kyle Nunas nchini Tanzania kuhusu ushirikiano wa kimakakati katika kuendeleza sekta ya madini kwa upande wa kufanya utafiti wa Jiofizikia yaani High Born Gegophysical Survey unaotumia ndege katika kupiga picha.

Mazungumzo hayo yamefanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere (JINCC) jijini Dar es salaam mapema baada ya mkutano huo kufunguliwa, akizungu mza juu ya hali halisi ya utafiti wa Jiofikizia nchini Tanzania, Mhe. Mavunde amesema kuwa mpaka sasa Tanzania imefanikiwa kufanya utafiti huo kwa asilimia kumi na sita (16%) kwa nchi nzima ambazo ndio zimeleta uwekezaji uliopo sasa.

Kwa upande wake Balozi Nunas amehaidi kutoa ushirikiano wa kikamilifu katika kuhakikisha jambo hilo linafanyika na kuiwezesha Tanzania kuwa na taarifa za kimakakati katika kuendeleza sekta ya madini nchini.

Mkutano wa Kimataifa wa Madini na Uwekezaji kwa mwaka 2023 unaendeshwa na kaulimbiu inayosema“ Bridging Tanzania’s Mining Sector to the World”.

SEKTA YA MADINI IMEENDELEA KUCHANGIA UCHUMI WA TANZANIA

Akielezea Mchango wa Sekta ya Madini katika kuchangia fedha za kigeni wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini Tanzania kwa Mwaka 2023, Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini Kheri Mahimbali amesema Kumekuwa na ongezo Kwa Thamani ya Madini yanayosafirishwa nje ya nchi kutoka Dola za Marekabi Bil. 3.1 kwa mwaka 2021 hadi kufika Dola Marekabi Bil 3.4 Kwa mwaka 2022.

Mahimbali ameongeza kwamba, kufuatia utekelezaji wa Sera ya Madini ya Mwaka 2009, kiasi cha manunuzi ya bidhaa za ndani katika miradi mikubwa kimeongezeka kutoka Dola bilioni 700 mwaka 2021 hadi kufikia Dola za Marekani trilioni 1.1 mwaka 2022.

Mafanikio hayo yamechochea sekta ya madini kukua kutoka asilimia 9.4 mwaka 2021 hadi kufikia asilimia10.9 mwaka 2022.

TGC YATAOA TUZO KUTHAMINI MCHANGO WA RAIS SAMIA, DKT. BITEKO SEKTA YA MADINI

Ikumbukwe tu Sekta ya Madini imeendelea kufanya vizuri kiuchumi ikijumuisha ukuaji wake, mchango wake katika maendeleo, uchumi na namnainavyochangia fedha za kigeni kutokana na nia dhabiti ambayoimeoneshwa na Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufuatia miongozo na maelekezo yake ambayo amekua akiyatoa kwa Wizara ya Madini.

Aidha, katika kipindi chote ambacho alikuwa waziri wa Madini, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Dkt. Doto Biteko, mchango wake katika kusimamia sekta ya madini umekua dhahiri. Kwa kulitambua hilo, wakati wa ufunguzi wa Mkutano waKimataifa wa Sekta ya Madini Mwaka 2023, Kituo cha Jemolojia Tanzania kilicho chini ya Wizara ya Madini kimetoa tuzo kwaviongozi haomkuthamini mchango wao katika sekta hiyo.

Akizungumza kuhusu tuzo hizo, Mratibu wa Kituo hicho Daniel Kidesheni amesema Tuzo ya Mhe. Rais Dkt. Samia metengenezwa kwa madini ya Zoisite (hornblende nyeusi na anyolite ya kijani), juu kuvalishwa kwa crown ya Silver na kito Cha Moldevite).

Ameongeza kuwa, "Mnara wa madini hayo unamaanisha kuwa Mhe. Rais anawaalika wawekezaji wote Duniani kuja kuwekeza nchini kwenye Sekta ya Madini na Sekta zingine," amesema Kidesheni.

Zawadi nyingine iliyotolewa ni ni bidhaa za sorana zilizotengenezwa kwa madini ya Silver na Amethyst (maana ya amethyst iaonesha symbolize deep love, happiness, Power and Wealth) ikimaanisha kuwa Mhe. Rais ana upendo na furaha kubwa kwa watanzania na watu wote duniani huku pia ikionesha utajiri wa rasimali Madini zinazopatikana nchini.

STAMICO YANADI FURSA ZA UWEKEZAJI MADINI MKUTANO WA MADINI

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Madini la Taifa, (STAMICO) Dk. Venance Mwasse ametoa wito kwa wawekezaji kutoka ndani ya nje ya nchi kuja kuwekezaji kutokana na mazingira rafiki yanayoendelea kuwekwa na serikali ya awamu ya sita chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan

Dkt. Mwasse ametoa kauli hiyo leo Jumatano tarehe 25 Oktoba 2023 wakati akichangia mada katika Mkutano wa kimataifa wa Madini na Uwekezaji Tanzania unaofanyiika jijini Dar es salaam.

Dkt. Mwasse amesema kutokana na jitihada zinazofanywa na Rais Dkt. Samia katika kuiboresha sekta ya madini, Shirika hilo kwa sasa limejengewa uwezo katika nyaja mbalimbali ikiwamo kuwa na Mitambo ya Kisasa ya uchorongaji wa miamba migodini. "Kwa hiyo ninawakaribisha sana tuje tushirikiane na kila mmoja atafaidika kulingana na mazingira bora yaliyowekwa, " amesema Dkt. Mwasse.

"Kwa sasa tunafanya kazi na Kampuni ya Anglogold Ashanti katika shughuli za uchorongaji wa miamba na tuna hisa katika umiliki katika mgodi mpya wa Dhahabu wa Buckreef ambao ulianzishwa mwaka jana na kwa sasa umekuwa chachu katika maendeleo ya sekta ya madini nchini," amesema.

Mkutano huo wa Siku mbili umenza leo tarehe 25 Oktoba 2023 na unaongozwa na Kauli mbiu isemayo "Unlocking Tanzania's Future Mining Potential". Kaulimbiu hiyo imelenga kuweka mazingira yatakayowezesha kuvuna madini yaliyopo Tanzania kwa manufaa ya kiuchumi na kijamii kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Mkutano huo umefunguliwa rasmi leo na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Dkt. Doto Biteko.

SERIKALI YAIMARISHA MIUNDOMBINU KURAHISISHA SHUGHULI ZA MADINI

Kutokana na umuhimu wa miundombinu mbalimbali katika kuwezesha shughuli mbalimbali nchini ikiwemo Sekta ya Madini kutokana na mchango wake katika kukuza uchumi, Serikali imeeleza kuwa inaendelea kuimarisha miundombinu ya usafirishaji ikiwa ni pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa na barabara zinazounganisha maeneo yenye migodi na shughuli mbalimbali za madini ili kurahisisha usafirishaji wa bidhaa zinazoingia na kutoka migodini.

Hayo yamebainishwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Dkt. Doto Biteko wakati akifungua Mkutano wa Kimataifawa Uwekezaji katika Sekta ya Madini Tanzania Mwaka 2023 na kueleza kuwa sasa Serikali inaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa barabara kutoka kijiji cha Paradiso hadi Kitai Mkoani Ruvuma yenye urefu wa kilomita 22 kwa kiwango cha lami na barabara ya Kabulo-Kiwira yenye urefu wa kilomita 7 mkoani Songwe kwa kiwango cha changarawe.

Dkt. Biteko ameeleza kwamba, barabara hizo zitakapokamilika zitarahisisha usafirishaji wa makaa ya mawe kutoka migodini kwenda kwa watumiaji wa ndani na nje ya nchi.

USHIRIKI WA WATANZANIA KATIKA UCHUMI WA MADINI WAONGEZEKA

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini Tanzania Mwaka 2023, Naibu Waziri Mkuu na Nishati Dkt. Doto Biteko kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, amesema takwimu zinaonesha kuwa fursa za ajira zimeongezeka katika sekta ya madini kutoka ajira 7,151 mwaka 2020 hadi ajira 16,462 mwaka 2022 sawa na ongezeko la zaidi ya mara 2 katika kipindi cha miaka mitatu kwa migodi mikubwa na ya kati pekee.

Akizungumzia shughuli za uchimbaji mdogo amesema zaidi ya watanzania milioni 1.5 wanashiriki katika shughuli za uchimbaji mdogo. Ameongeza kwamba, ununuzi wa bidhaa za ndani umeongezeka kutoka manunuzi ya dola za Marekani milioni 715.3 mwaka 2019 hadi dola za Marekani trilioni 1.1 mwaka 2022.

"Hii inaonesha namna Sekta ya Madini ilivyokuwa muhimu katika uchumi wa nchi yetu," amesisitiza Dkt. Biteko.

Migodi Mikubwa, Midogo Yafikiwa na Nishati ya Umeme

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Dkt. Doto Biteko akizungumza kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini amesema sasa baadhi ya migodi mikubwa ikiwemo Geita Gold Mines Limited (GGML) na STAMIGOLD Biharamulo Mine ambayo ilikuwa haina umeme kwa muda mrefu sasa imeunganishwa na umeme wa gridi ya Taifa. Ameongeza kwamba

migodi zaidi ya 350 ya wachimbaji wadogo imeunganishwa na umeme wa gridi ya Taifa na hivyo kupunguza gharama za uzalishaji na kurahisisha shughuli mbalimbali za migodi. Serikali inafahamu kuwa bado kuna mahitaji makubwa ya migodi kuunganishwa na umeme wa gridi ya Taifa.

" Napenda kuwahakikishia kuwa, kadri tunavyoimarisha uwezo wetu wa kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme nchini, tutahakikisha migodi yote mikubwa na midogo inaunganishwa na umeme wa gridi ya Taifa," amesema.

MKUTANO WAKUTANISHA WADAU WAPATAO 2,000

Akizungumza katika mkutano-huo, mwandaaji Mwenza Mkurugenzi wa Kampuni ya Ocean Business Partners, Balozi Abdul-Samad amesema mkutano huo umewakutanisha washiriki wapatao 2,000 kutoka Mataifa mbalimbali Duniani ikiwemo Vietnam, Australia, Thailand, Burundi, Uganda na mengine

Ameongeza kwamba, mkutano huo imelenga kubadilishana uzoefu, kutangaza mnyororo mzima wa shughuli za madini na kuongeza kwamba ni jukwaa lenye manufaa kwa Tanzania. Kwa upande wake, mwandaaji Mwenza Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya dmg Events ya nchini Uingereza Damian Howard ameishukuru Serikali Kwa kukubali kushirikiana na kampuni hizo kuandaa mkutano huo.

www.madini.go.tz

Ministry of Minerals,
Madini Street,
Government City - Mtumba
P. O. Box 422,
Dodoma 21207, Tanzania
Email: ps@madini.go.tz